

Toni katika vitenzi vya kimochi

Clarah Nelson

M. A. (Kiswahili)

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Kiswahili, 2013

Tasnifu hii imelenga kuelezea utafiti uliochunguza “Toni katika Vitenzi vya Kimochi” kwa kutumia kiunzi cha nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru katika uchanganuzi wa data. Nadharia hii iliasisiwa na Goldsmith (1976) ambapo vipengele vya kifonolojia vimewakilishwa katika rusu huru. Utafiti huu umegusia vipengele vya kifonolojia kama vile irabu, konsonanti, silabi na michakato ya kifonolojia inayoathiri ruwaza za toni. Data zilizotumika katika utafiti huu ni vitenzi visoukomo vilivyokusanywa uwandani katika vijiji vya Tsuduny, Shia, Kidia, Mowo na Mbokomu vilivyoko katika Kata ya Old-Moshi Mashariki, Wilayani Moshi vijini, Mkoa wa Kilimanjaro. Data zilikusanywa kwa hojaji, mahojiano na kurekodiwa kwa kinasasauti aina ya *MP3 IC recorder* na kuchambuliwa kwa mbinu ya uchanganuzi wa data kimada. Imebainika kuwa toni za lugha hii ni tabirifu ambapo kitenzi huanza na tonichini katikati tonijuu na mwisho tonichini. KTM ni CJC. Utokeaji wa toni katika vitenzi visoukomo vya lugha hii hutegemea idadi ya silabi za shina la kitenzi. Kiinitoni katika vitenzi visoukomo huangukia katika silabi ya mwisho kasoro moja. Na kiinitoni hicho kinahusishwa na tonijuu ya KTM.